**MAPENDEKEZO YA VIPAUMBELE VYA WIZARA KWA MWAKA 2026/27**

**A. Kuendelea na utekelezaji wa Sera na Mitaala, Mapitio ya Sheria, Kuandaa Miongozo na Kutoa Mafunzo Nchini**

i. Kuendelea na uandaaji wa zana za utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo 2014, Toleo la 2023 ikiwemo Mfumo wa Taifa wa Mitaala (National Curriculum Framework) na kukamilisha Mfumo wa Taifa wa Upimaji na Tathmini (National Assesment Framework) na Mwongozo wa kubaini na kuendeleza vipaji na vipawa katika ngazi mbalimbali za elimu;

ii. Kukamilisha mapitio ya Sheria ya Elimu, Sura 353 na sheria tisa katika taasisi ambazo ni COSTECH, TLSB, NECTA, TEWW, VETA, TCU, NACTVET, TIE na TEA ili ziendane na Sera ya Elimu na Mafunzo ya 2014, Toleo la 2023 na Sheria za Kikanda na Kimataifa;

iii. Kuanzisha Bodi ya Kitaalamu ya Walimu Tanzania (Tanzania Teachers Professional Board) ili kusimamia, kudhibiti na kuunda taaluma ya ualimu nchini;

iv. Kufanya tathmini ya utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo 2014, Toleo la 2023 na mitaala ya elimu;

v. Kuendelea na maboresho ya mitaala ngazi ya elimu ya Amali (Ufundi na Mafunzo ya Ufundi stadi) na Elimu ya juu kwa lengo la kuimarisha ujuzi kwa wahitimu wa ngazi hizo;

vi. Kuwezesha maandalizi ya Kundi rika mbili (double cohort) kwa ajili ya kupokea wanafunzi darasa la 6 na la saba kwa wakati mmoja) kwa Jan 2028;

vii. Kutekeleza mpango wa wahitimu wa mafunzo ya ualimu kufanya mazoezi ya kufundisha kwa vitendo kwa muda wa mwaka mmoja (‘Internship’);

viii. Kuendelea kutoa elimu kwa umma na watendaji kuhusu Sera ya Elimu na Mafunzo 2014,Toleo la 2023 na mitaala kwa ngazi ya Elimu ya Msingi, Sekondari, Ualimu, Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi na Elimu ya Juu;

ix. Kukamilisha mapitio ya Sera ya Sayansi na Teknolojia (1996) ili kuwa na sera inayoakisi hali halisi na mahitaji ya sasa katika Sayansi, Teknolojia na Ubunifu;

x. Kukamilisha mapitio ya Muundo na Majukumu ya Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia kwa lengo la kuimarisha ufanisi na mchango wa Sayansi, Teknolojia na Ubunifu katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii; na

xi. Kuwezesha vyuo vya elimu kufanya mafunzo ya ulezi (Mentorship) ili kukuza vijana kwenye uongozi.

**B. Kuongeza Fursa na Kuimarisha Ubora wa Mafunzo ya Amali katika shule za Sekondari na Vyuo vya Amali**

i. Kuendelea kuimarisha Kampasi ya Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mtwara;

ii. Kuimarisha upatikanaji wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia hususani vifaa vya amali na vitabu vya kiada kufikia uwiano 1:1;

iii. Kuwezesha uanzishaji wa programu maalum katika vyuo vya mafunzo ya ufundi Stadi zitakazounganishwa na miradi ya kimkakati nchini;

iv. Kuendelea kuwezesha ujenzi wa VETA katika Wilaya 64 na Kimoja cha Mkoa wa Songwe;

v. Kununua vifaa vya kufundishia na kujifunzia katika Vyuo vya VETA 145, FDC 55 na Vyuo vya ufundi stadi na Marekebisho wa watu wenye mahitaji maalum;

vi. Kuwezesha ujenzi wa miundombimu mipya na ukarabati wa majengo ya Vyuo tisa (9) vya ufundi stadi na Marekebisho kwa watu wenye mahitaji maalum;

vii. Kuanza utekelezaji wa Mfumo wa Taifa wa Sifa Linganifu (Tanzania National Qualification Framework);

viii. Kuwezesha ujenzi wa vyuo vitano (5) vya ufundi (Polytechnics college); na

ix. Kuendelea kuboresha vituo vya umahiri kwa ajili ya kuimarisha utoaji wa mafunzo ya fani za kipaumbele kupitia Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam, Chuo cha Ufundi Arusha Chuo cha Taifa cha Usafirishaji na Kituo cha Magonjwa ya Moyo – Mloganzila.

**C. Kuongeza Fursa na Kuimarisha Ubora wa Elimu ya Awali, Msingi, Sekondari, Ualimu na Vyuo vya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi**

i. Kuimarisha Udhibiti ubora wa elimu kupitia SQA na NACTVET kwa kuwezesha ufanyikaji wa Tathmini ya Jumla ya Ubora;

ii. Kuandaa na kutekeleza mkakati wa kitaifa wa Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK);

iii. Kuendelea kutoa mikopo kwa wanafunzi wa Stashahada kutoka 17,420 mwaka 2025/26 hadi kufikia 27,200 mwaka 2026/27 katika fani za sayansi na ufundi;

iv. Kuendelea kuimarisha mafunzo kazini na tarajali kwa walimu, wakufunzi na wasimamizi wa elimu nchini;

v. Kuendelea kuimarisha uwiano wa kitabu kimoja kwa mwanafunzi katika ngazi ya elimu ya msingi na sekondari pamoja na kuimarisha huduma ya maktaba za jamii kwa ununuzi wa vitabu;

vi. Kuendelea kuimarisha utoaji wa elimu maalum na jumuishi kwa walimu na wanafunzi wenye mahitaji maalum ikiwa ni pamoja na kuimarisha huduma ya ubainishaji na upimaji na utoaji wa elimu nyumbani kwa wanafunzi wenye magonjwa adimu, uandaaji wa miongozo kwa ngazi zote za elimu; na

vii. Kutoa ufadhili wa masomo kwa walimu 1,223 watakaosoma Diploma ya Ualimu wa Elimu Maalum.

**D. Kuongeza Fursa na Kuimarisha Ubora wa Elimu ya Juu**

i. Kuongeza fursa za mikopo kwa wanafunzi wa Elimu ya Juu kutoka 252,773 mwaka 2025/26 hadi wanafunzi 325,645 (mwaka wa kwanza 105,450 na wanaoendelea 220,195) kwa mwaka 2026/27;

ii. Kuwezesha utekelezaji wa program ya Samia Extended Scholarship (DS/AI +) kwa kutoa ufadhili kwa wanafunzi wenye ufaulu wa juu wa masomo ya Sayansi katika matokeo ya Kidato cha Sita kutoka wanafunzi 50 mwaka 2025/26 hadi wanafunzi 100 (mwaka wa kwanza 50 na wanaoendelea 50) ili kujiunga na Shahada ya Kwanza katika vyuo bora vilivyo nje ya nchi kusomea mambo ya kompyuta na akili-unde;

iii. Kuendelea kuwezesha ufadhili katika eneo la sayansi na teknolojia ya nyuklia kwa shahada ya umahiri;

iv. Kuendelea kutoa ufadhili kwa wanafunzi wenye ufaulu wa juu katika masomo ya Sayansi, teknolojia, uhandisi na hisabati (STEM) kupitia SAMIA Skolashipu kutoka wanafunzi 2,630 mwaka 2025/26 hadi wanafunzi 3,475 mwaka 2026/27 (wanafunzi 1,000 wa mwaka wa kwanza na wanafunzi 2,475 wanaoendelea);

v. Kuandaa Mpango Mkuu wa Elimu ya Juu 2026-2030 (Higher Education Master Plan 2026 – 2030) wa kuwezesha vyuo vikuu kuwa na umahiri unaojipambanua katika nyanja za kipekee (prestigious Universities);

vi. Kuendelea kugharamia mafunzo kwa wanataaluma katika ngazi ya umahiri na shahada ya uzamivu katika fani mbalimbali katika vyuo vikuu nchini; na

vii. Kumalizia ujenzi na ukarabati wa miundombinu katika kampasi 16 za taasisi za elimu ya juu.

**E. Kuimarisha Uwezo wa Nchi katika Utafiti, Matumizi ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu ili Kuchochea Ujenzi wa Uchumi wa Viwanda**

i. Kuimarisha ushiriki wa sekta ya umma na binafsi katika kuongeza mchango wa utafiti na ubunifu kwenye maendeleo ya kiuchumi na kijamii;

ii. Kuongeza uwekezaji katika miundombinu ya kitaifa ya utafiti na ubunifu ili kuchochea uvumbuzi na ubiasharishaji wa teknolojia zinazoibuliwa nchini;

iii. Kuendelea kutoa tuzo kwa watafiti watakaochapisha matokeo ya utafiti katika majarida yenye hadhi ya juu kimataifa;

iv. Kuendelea kuhamasisha Taasisi za Elimu ya Juu na Taasisi za Utafiti na Maendeleo kufanya tafiti za kimkakati katika sekta zenye mchango mkubwa kwenye kukuza uchumi na kuboresha maisha ya jamii;

v. Kuendelea kuimarisha matumizi ya TEHAMA na teknolojia za kidijitali katika ujifunzaji na ufundishaji kwa ngazi zote za elimu nchini;

vi. Kuimarisha Mfuko wa Ubunifu wa Samia (Samia Innovation Fund) ili kuongeza idadi ya bunifu na teknolojia zinazoendelezwa na kuingia sokoni;

vii. Kuimarisha uthibiti na utafiti wa kimkakati unaolenga kuongeza wigo wa matumizi salama ya teknolojia ya nyuklia katika sekta mbalimbali za kiuchumi na kijamii; na

viii. Kukamilisha maandalizi ya Taifa ya Mahitaji ya Teknolojia katika sekta mbalimbali (National Technology Roadmap-2050).